

## **NEEMA TULIYOTUNUKIWA**

Inawezekana jamii imesahau kuwa katika kuleta maendeleo kwenye jamii nguvu kazi inahitajika kwa kutumia rasilimali tulizonazo ili kuweza kufikia malengo ya serikali ya awamu ya tano ya uchumi wa viwanda.

Miongoni mwa rasilimali hizo muhimu ni uvuvi na ufugaji, ambazo zinaweza kutoa ajira mbalimbali kwa vijana na jamii kwa ujumla hasa katika maeneo yapatikanayo karibu na vyanzo vya maji kama vile bahari, maziwa, mito na mabwawa.

Nchi yetu Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizo barikiwa sana kwa uwepo wa rasilimali hizo ambazo zingetegemewa kutoa mchango mkubwa katika pato la taifa na maendeleo kwa ujumla. Tanzania ina ng'ombe wanaokadiriwa kufikia milioni 22.8, Mbuzi milioni 15.9, Kondoo milioni 7, Kuku wa asili milioni 35.5 na Kuku wa kisasa milioni 24.5.

Hata hivyo idadi hii ya mifugo kwa muda mrefu haijatoa mchango unaotakiwa katika pato la Taifa kutokana na wafugaji wengi kufuga kwa njia ya asili.

Kulingana na takwimu zilizotolewa na ofisi ya Taifa ya Takwimu mwaka jana, sekta ya mifugo inakuwa kwa asilimia 3.8 na kuchangia asilimia 4.4 ya pato la Taifa. Naibu waziri Telele anasema kwa sasa kuna ng'ombe wa nyama wenye uzito wa kufikia kilo 1000 ambapo kwa bei ya Sh.3000 kwa kilo, mnyama hai ana thamani ya Sh.milioni 3.

Ukweli huu haujaakisiwa kwa vitendo kwa kuwa jamii inajisahau kutoa kipaumbele katika shughuli hizo nakuona kwamba ni zakufanywa na watu la tabaka la chini na wasiokuwa na elimu, la hasha!

Shughuli hizi ni muhimu sana katika kujiletea maendeleo na kupunguza wimbi la ukosekanaji wa ajira kwa vijana unao pelekea maovu mbalimbali katika jamii kama vile wizi, ubakaji, matumizi ya madawa ya kulevya na uwajibikaji.

Mkoa wa Mara ni miongoni mwa mikoa ya kanda ya ziwa ambapo fursa hizi zinapatikana kutokana na uwepo wa ziwa Victoria, mto Mara na mabwawa mbalimbali pamoja na uwepo wa maeneo makubwa ya malisho.

Miongoni mwa wilaya za mkoa wa Mara zinazotekeleza shughuli za ufugaji na uvuvi ni pamoja na Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ambapo idara ya mifugo na uvuvi ina watumishi 12 watumishi 2 wapo makao makuu ya halmashauri wakisimamia na kufutulia shughuli zinazo tekelezwa na idara.

Aidha, watumishi 10 wamepangwa katika ngazi ya Kata kwa ajili ya kutoa huduma za ugani ambapo sekta ya mifugo ina watumishi 7 na sekta ya uvuvi ina watumishi 3.

Idara ina mahitaji ya watumishi 33 na upungufu wa watumishi 21 ikiwa ni mojawapo ya changamoto katika sekta hii.

## **Mifugo**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2015/2016 hadi Mei 2018 sekta ya mifugo imetekeleza shughuli mbalimbali kama vile kutoa elimu ya ufugaji bora kwa mifugo mbalimbali ndani ya Manispaa kwa wafugaji 254, kutoa huduma ya juu ya uzalishaji wa ngombe wa maziwa kwa njia ya chupa kwa wafugaji 98 wa ng'ombe wa maziwa.

Vilevile mafunzo ya uboreshaji wa kuku wa asili na kuwezesha kununua majogoo bora 300 ya kuku kwa vikundi vya wafugaji wa kuku na kwa mfugaji mmoja mmoja.

Pamoja na utambuzi wa magonjwa, ufuatiliaji, utoaji kinga na tiba, mifugo 170,685 ilipatiwa chanjo mbalimbali kwa miaka mitatu ili kuikinga na magonjwa anuai kama vile kideri cha kuku, ndui ya kuku, kichaa cha mbwa na paka, ugonjwa wa mapele ya ng'ombe na mbuzi.

Pia kusimamia na kutekeleza sheria ya magonjwa ya mifugo ya mwaka 2013 kwa kufanya uchaguzi wa awali wa mifugo ambayo ni ng'ombe,mbuzi na kondoo, pamoja na kusimamia nakufatilia mapato ya Halmashauri yanayotokana na chanzo cha machinjio.

Hata hivyo, katika kukabiliana na changamoto hizo Halmashauri ya Manispaa ya Musoma kupitia idara imeshauri serikali iongeze bajeti ya sekta ya mifugo na uvuvi,Halmashauri kuendelea kuomba kibali cha kuajili maafisa ugani,kuwekeza kwenye uwendelezaji wa zao la ngozi na mazao mengine ya mifugo.

## **UVUVI**

Katika kusimamia na kutekeleza sera ya sheria ya uvuvi namba 22 ya mwaka 2003 pamoja na kanuni zake za mwaka 2009 zinahimiza kuachana na uvuvi haramu na kuendeleza uvuvi endelevu.

Halmashauri inajihusisha kuhamasisha na kutoa elimu juu ya ufugaji bora wa samaki kwa wadau mpaka sasa imewafikia wadau 223. Aidha hadi sasa mabwawa ya samaki yaliyopo ni 33 ,baadhi ya mabwawa kati ya hayo yamepandikizwa samaki aina ya sato na mumi ambapo yote yapo katika hatua tofauti za uzalishaji.

Pamoja na mikakati hiyo idara inakabiliana na changamoto mbalimbali kama vile kushidwa kutekeleza baadhi ya miradi mbalimbali ya maendeleo mfano huduma ya uhamilishaji,ununuzi wa chanjo mbalimbali za magonjwa ya mifugo n.k

Hali kadhalika upungufu wa watumishi katika kutekeleza shughuli za ugani ngazi ya Halmashauri na kata kwani mahitaji ni 33 na watumishi waliopo ni 12, ukosefu wa vitendea kazi hususani boti na injini katika kupambana na uvuvi haramu na kukusanya mapato ya Halmashauri.

Hivyo basi, katika kuboresha sekta ya ufugaji na uvuvi serikali iongeze bajeti ya sekta hiyo na pia Halmashauri kuendelea kuomba kibali cha kuajili maafisa ugani nakuwekeza kwenye uendelezaji wa zao la ngozi na mazao mengine ya mifugo.

Ili kuendana na sera ya uchumi wa viwanda katika kufikisha nchi yetu kwenye uchumi wa kati sekta binafsi na jamii kwa ujumla inapaswa kushirikiana na serikali katika kufikia malengo hayo endelevu na kutokomeza wimbi la umaskini linalokabili nchi yetu.